# Nani? Doris Day?

Ngurumo 15/2/63

"Habari iliyotolewa katika gazeti lako la tarehe 8th February No. 1,179," yamsema Doris Day.

Nani? Kama ni yeye Doris Day, basi huyo kijana wa Frelimo sio wa Frelimo tena, kwa kuwa Frelimo imemtolea radhi basi yeye si kijana wa Frelimo, hata huko Cairo hakai katika nyumba ya Frelimo la, yeye sasa maisha yake na Doris Day wake ni kutapa tapa tu.

Twasikia kuwa sasa Doris Day hana furaha kama zamani, ah! hiyo ni hiyari yake, kwa kuwa asiyesikia la mkuu atavunjika mguu, yeye alipatwa na tamaa ya 'I lavu yu bibi' basi akaona vya bure tu kumbe Cairo sio Tanganyika baba, ama sio watachimba mbuyu huko, kama hakuna poketi fulu basi ......watakiona.

Hata huyu kijana aitwaye ...... nami jina nimelikumbatia lisianguke, atajutia na uhalifu wake. Watu husema 'cha mtu mavi ukikiona kiteme mate' basi hayo tena.